| Mary Wanjiru Watheka & Isaiah Ngotho Watheka | Keziah Wanjiku Watheka | Absa Bank of Kenya |
| George Gitua Wamwea & Ruth Njoki Muthumbi | Josephat Wamwea Gathii | Sameer Group |
| Harriet Nzula Mathew | Mutungi Paul Musembi | Bank of Africa Kenya Ltd |
| Stephen Kinyanjui Ngugi | Ngugi Isabella Gathoni Moses | Standard Chartered Bank |
| Ruth Njeri Gachwe | Samuel Gachue Mbugua | British American Tobacco |
| Mary Wanjiku Gichuhi | Peter Gichuhi Mwaniki | Carbacid Investments Plc |
| Andrew Oboch Nyandong & Leonida Were Otieno | Margaret Auma Nyandong | Absa Bank of Kenya |
| Thomas Abwodha Roche & Collins Maurice Otieno Tuju | Damar Ayiemba Roche | East African Breweries Ltd |
| Pauline Moraa Kinyanjui | James Kinyanjui Kiarie | Safaricom Plc |
| James Kihiu Munge | Munge Karanja Munge | Co-operative Bank of Kenya |
| Wanja Kamau | Francis Ndung'u Kariuki | Safaricom Plc |
| Brenda Wanjiru Waweru & Jane Wambui Kimani | Tabitha Wangui Gacheru | Safaricom Plc |
| Vincent Odhiambo Ondiwo & Grace Akinyi Ondiwo | James Ondiwo Opande | Co-operative Bank of Kenya |
| Mdhamini wa Umma– Machakos | Nzulu Ndolo | British American Tobacco |
| Mdhamini wa Umma - Machakos | Johnson Kinyua Kamau | KCB Group Plc |
| Wilson Ngatia Mwai, Jane Wangui Mwai & George Wambugu Mwiki | Wambugu Mwai | NIC Bank |
| Public Trustee- Nairobi | Mwituria John Ngunjiri Isaac | Absa Bank Kenya Plc |
| Public Trustee- Nakuru | Peris Wanja Njoroge | Safaricom Plc |
| Prisca Achieng Ochieng | Antipas Ochieng Ojwaya | Co-operative Bank of Kenya |
| Deputy County Commissioner - Kesses | Martha Kabura Waweru | Equity Bank Kenya Ltd |
| Mdhamini wa Umma - Nairobi | Stephen Nduti Ngotho | Safaricom Plc |
| Naibu Mdhamini wa Umma - Kakamega | Rose Ndovola Akamo | KCB Group Plc |
| Mdhamini wa Umma - Nyeri | Jonah Kamau Githui | NIC Bank |
| Esther Waithira Karu | Karu Wilson Kariuki | KCB Group Plc |
| Patrick Peterson Maimba & Emma Wanjiru Wanyoike | Harrison Wanyoike Maimba | Standard Chartered Bank |






A

| Jina la Mlalamishi/ Msimamizi | Jina la Mmiliki Halisi/ Marehemu | Mshikilizi |
|---|---|---|
| Mdhamini wa Umma - Nyeri | Charles Kariuki Mathenge | Kenya National Assurance ltd |
| Catherine Wanjiru Mwangi | Pierre Kamau Mwangi | Co-operative Bank of Kenya |
| Subjali Kassam Hassam Bhanji | Abdulla Hassam Bhanji | Jubilee Insurance Company |
| Mahebub Fazal Rajani | Fazal JanMohamed Rajani | Diamond Trust Bank |
| Public Trustee - Nyeri | James Magethe Rukahu | Safaricom Plc |
| Teresa Osebe Makori | Andrew P Makori Ong'ou | Standard Chartered Bank |
| Caroline Nazi Karisa, Samuel Kitsao Karisa & Rachael Karisa | Fondo John Karisa | HFC Group |
| Samuel Mwangi Mwithiga & Charles Chege Mwithiga | Ezakiel Muithiga Kingangi | Standard Chartered Bank |
| Susan Wanjiru Kiruma & Anne Njoki Wanjohi | Kiruma Peter Waweru | Kenya National Assurance Ltd |
| Deputy County Commissioner - Nairobi | John Kagoiya Kamuri | Consolidated Bank of Kenya |
| Patrick Ng'ang'a Wairimu | Esther Wanjiru Kariuki | KCB Group Plc |
| Public Trustee - Nairobi | Jane Wangui Kimondo | Absa Bank of Kenya |
| Mdhamini wa Umma - Machakos | Stanley Gatimu Munge | East African Breweries Ltd |
| Margaret Atieno Owuor | Japheth Owuor Ondiek | Kenya National Assurance |
| Public Trustee - Nairobi | Nancy Njeri Nduati | KCB Group Plc |
| Public Trustee - Nairobi | Francis Gakuru Njura | KCB Group Plc |
| Public Trustee - Machakos | Makuthi Mwikya Muthoka | Standard Chartered Bank |
| Public Trustee - Eldoret | Martin Tormoi Too | Standard Chartered Bank |

## KUPOTEZA BIMA

Notisi inatolewa kwa mujibu wa kanuni ya 9 ya Kanuni za Raslimali za Kifedha Zisizodaiwa za mwaka 2016 ambazo Mamlaka ya Mali Zisizodaiwa imepokea madai ya mali ambayo haijadaiwa kutoka kwa watu ambao, kupitia viapo vya kiapo, wameonyesha kuwa nyaraka za awali za bima zimepotea.

| Jina la Mlalamishi | Namba ya Bima na Mshikilizi wa Bima | Jina la Kampuni ya Kutoa Bima |
|---|---|---|
| Bethy Mumbi Njenga | Bethy Mumbi Njenga – 020/EAW/011597 | ICEA Lion Life Assurance Ltd |

Taarifa zaidi inatolewa kwamba isipokuwa tu pingamizi la madai litawasilishwa katika ofisi za Mamlaka kwa anuani iliyo hapa chini ndani ya siku thelathini (30) kuanzia tarehe hii, malipo yatafanywa kwa watu waliotajwa hapo juu kwa ushahidi wa kiapo cha kupotea kwa hati asili ya sera na dhima yoyote kwenye hati ya sera iliyopotea itakoma mara moja.

Mamlaka ya Mali Zisizodaiwa, Kituo cha Pacis, Orofa ya 2, nje ya Waiyaki Way, P. O. Box 28235 - 00200, Nairobi.

**F.A JOHN MWANGI, EBS**
**AFISA MKUU MTENDAJI & MDHAMINI MKUU**

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA

nema

**NATIONAL ENVIRONMENT MANAGEMENT AUTHORITY**

**Popo Road, off Mombasa Road P.O. BOX 67839-00200, Nairobi, Kenya**
**Tel: (254 020) 6005522, 6001945, Fax: (254 020) 6008997) E-mail: dgnema@nema.go.ke, Website: www.nema.go.ke**

## NOTICE TO THE PUBLIC TO SUBMIT COMMENTS ON AN ENVIRONMENTAL IMPACT ASSESSMENTSTUDY REPORT FOR THE PROPOSED REHABILITATION AND EXTENSION OF WATER SUPPLY NETWORK WITHIN KISUMU CITY AND SATELLITE TOWNS- WORKS PACKAGE 2 LOT 1

Pursuant to Regulation 21 of the Environmental Management and Coordination (Impact Assessment and Audit) Regulations, 2003, the National Environment Management Authority (NEMA) has received an Environmental Impact Assessment Study Report for the above proposed project.

The proponent **Lake Victoria South Water Works Development Agency (LVSWWDA),** proposes to rehabilitate, reinforce and extend water supply infrastructure in Kisumu City to reduce Non-Revenue Water (NRW), Improve water supply within Northern and Eastern Kisumu through laying of secondary distribution network from Kajulu WTP, Mamboleo, Kibuye, Obwolo and Kanyamedha tanks; and rehabilitation and extension of water supply to adjacent localities including Kiboswa and Maseno. The project will be done in clusters within Kisumu City, Maseno and Gee areas. The scope of work will involve rehabilitation and extension of 156.7km (118Km OD63 to OD450, 25.7Km OD63 to OD200 and 13Km OD90 to OD 225) and will be within Kisumu City and Satellite towns under Works Package 2 lot 1.

The following are the anticipated impacts and proposed mitigation measures:

| Impact | Mitigation Measures |
|---|---|
| **Disruption of socio-economic activities within the project alignment areas** | • Business owners who have constructed their business premises within road reserves will be advised in advance to remove the structures before commencement of excavation activities.<br>• The affected traders will be compensated for loss of revenue during the period of interruption.<br>• Authorization to Work within road corridors shall be sought from relevant road authorities including Kenya national Highways authority, Kenya Urban Roads Authority (KURA), Kenya Rural Roads Authority (KeRRA) |
| **Disruption of services within the project alignment area** | • The contractor shall liaise with Kisumu Water and Sanitation Company (KIWASCO) and private water service providers to restore water services as soon as pipe laying and backfilling of trenched areas are finalized<br>• The contractor shall liaise with other service providers including Kenya Power Company and mobile/ fiber companies to restore power and telecommunication /fiber cables cut during excavation activities as soon as pipe laying and backfilling of trenched areas are finalized |
| **Labor Influx** | • Laborers from the local neighborhood will be given first priority during recruitment processes to mitigate influx of labor from outside the project area. |
| **Blockage of drainage channels** | • The contractor shall prepare spoil management plan before commencement of construction works which will spell out how spoils management will be achieved during construction period<br>• Stockpiling of materials will be done at least two (2) meters away from drainage channels and water courses. |
| **Impacts of obtaining construction materials** | • All new quarry and borrow pits opened for purposes of being sources of materials for the proposed project will be subjected to ESIA study in compliance with applicable laws, regulations and standards<br>• The contractor shall maximise the re-use of excavated materials in the works |
| **Accidents and Injuries to workers** | • The contractor shall prepare construction Environmental and Social Management Plan (C-ESMP) within 30 days after signing the contract to guide implementation of health and safety requirements during construction period.<br>• The contractor shall provide ample warning signs, guard rails, warning tape, etc.<br>• All persons handling equipment and materials shall be suitably trained, supervised and adequately instructed.<br>• Procedures and traffic controls, such as establishment of work zones so as to separate workers from traffic and from equipment as much as possible. |
| **Traffic Impacts** | • Traffic signs shall be erected within work areas to warn the public and motorists of the heavy/construction vehicles accessing the site. |
| **Risks to local residents** | • A HIV/AIDS prevention programme specific to the project's construction phase shall be established and implemented by the project proponent and contractor.<br>• The health and safety Officer who will be in charge of sensitization of workers on Covid 19 shall be stationed at the construction sites. S/He will create awareness amongst site personnel on COVID-19 throughout project construction period . |
| **Solid waste generation** | • The contractor will prepare a waste management plan at the start of construction activities which will spell out how solid wastes of various categories shall be managed.<br>• Express condition shall be put in the contract that before the contractor is issued with a completion certificate; they will clear the site of all debris and restore it to a state acceptable to the supervising architect and environmental consultant;<br>• The project proponent and the contractor shall engage a NEMA registered solid waste handling company to manage all solid wastes associated with the construction process. |
| **Soil erosion** | • The contractor shall prepare erosion and sedimentation plan before commencement of construction works which will guide management of erosion issues at the site; |
| **Dust Pollution** | • The project proponent and the contractor shall prepare air quality management plan before commencement of the works. The plan will spell out how air quality issues will be managed throughout construction period. |
| **Noise Pollution** | • The project proponent and the contractor shall prepare noise management plan before commencement of the works. The plan will spell out how noise pollution will be managed throughout construction period.<br>• Silencers on equipment such as generators will be properly designed<br>• Where need be, all exposed workers will be provided with functional ear muffs, whose use shall be mandatory and closely enforced, monitored and supervised. |
| **Water supply disruption** | • Consumers will be given advance warning ahead of water disruptions to enable them store water in quantities that can last them for the period of disruption;<br>• Kisumu Water and Sanitation Company (KIWASCO) shall be notified of any planned disruptions in writing to enable then disconnect water services ahead of excavation works.<br>• Water services shall be restored within 24 hours. |

The full report of project is available for inspection during working hours at:

1. Principal Secretary, Ministry of Environment and Forestry, NHIF Buildilng, 12th Floor, Ragati Road, Upper Hill P. O. BOX 30126 -00100, **NAIROBI**
2. Director General NEMA, Popo Road, Off Mombasa Road P.O. BOX 67839-00200, **NAIROBI**
3. County Director of Environment **KISUMU COUNTY**

A copy of EIA report can be downloaded at **www.nema.go,ke**

**NEMA** invites members of the public to submit oral or written comments within 30 days from the date of publication of this notice to the Director General, NEMA to assist the Authority in the decision making process for this project. Kindly quote **Ref. No. NEMA/EIA/5/2/2056.**

Comments can also be emailed to **dgnema@nema.go.ke**

**DIRECTOR GENERAL**

***This advertisement is sponsored by Lake Victoria South Water Works Development Agency***

KENYA VISION 2030 NemaKenya www.nema.go.ke

KOMESHA COVID-19
" Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa"
HOMA
KIKOHOZI
KUSHINDWA KUPUMUA
MAUMIVU KOONI
KUUMWA NA KICHWA

# Canada yatumia Sh 4.7b kwa mafunzo ya kiufundi

NA SAMUEL MAINA (KNA)

Serikali ya Canada imetumia zaidi ya Sh4.7 bilioni kufadhili mipango ya mafunzo ya kiufundi kama njia kubuni nafasi za kazi kwa vijana nchi Kenya.

Sehemu ya pesa hizo zimetumika kwa mipango ya kuwezesha wanawake kwa kulenga ukuzaji wa ujuzi na ujasiriamali kusaidia kupunguza viwango vya umasikini miongoni mwa wanawake.

Balozi wa Canada nchini Kenya Christopher Thornley alisema kwamba serikali yake inafanya kazi na vituo vya Elimu ya Kiufundi na Mafunzo Anuai (TVETs) nchini kuviwezesha kutoa mafunzo bora na yanayostahili kwa soko la ajira la kisasa.

Thornley alisema hayo katika Chuo cha Ufundi cha Kitaifa cha Nyeri alipokabidhi vifaa vya kisasa vya kutengeneza maziwa vilivyotolewa na

Canada chini ya Mpango wa Elimu Kenya kwa Ajira (KEFEP).

"Mradi huu (KEFEP) unasaidia kujenga mahitaji thabiti ya ongezeko la viwanda kutoa vifaa na ushirikiano unaoleta kazi kwa vijana wanaotoka vyuoni.

"Kwa sababu ya hii, serikali ya Canada imewekeza karibu dola

50 milioni kwa mipango iliyochaguliwa ya kukuza ujuzi ili kuchangia kwa malengo ya maendeleo endelevu yanayoonyesha kupunguza umasikini," alisema.

Balozi huyo alisema kwamba kwa kuwa vijana wanachangia asilimia kubwa ya wafanyakazi wanaohitajika nchini, kuna haja ya kuendelea kuwekeza katika TVET mama njia moja ya kuweka nchi katika tapo la nchi zilizoendelea.

Alisema kwamba kwa kushirikiana na taasisi za mafunzo nchini, Canada inaonyesha kujitolea kwake kutumia ujuzi wa vijana katika kuendeleza ajenda ya maendeleo inayotambua ujuzi wa kiufundi kama ulio muhimu katika kubadilisha hali ya kiuchumi ya nchi.

"Mradi huu unaonyesha kujitolea kwa Canada katika kuendelea kusaidia jukumu la Kenya la kupanua mafunzo ya kiufundi kujenga ujuzi wa vijana na pia kuchangia kuunda ajira na kuharakisha ukuaji wa uchumi kulingana na ajenda yake ya maendeleo na kubadilisha Kenya kuwa nchi ya viwanda ya mapato ya kati," alisema.

"Vifaa vilivyotolewa ni muhimu na vinatoa ujuzi unaohitajika kwa wanafunzi chini ya muundo wa mafunzo wa Umilisi na Utendaji," aliongeza.



**Balozi wa Canada Kenya, Christopher Thornle (kulia) Gavana wa Nyeri, Mutahi Kahiga (kati) na Katibu wa Mafunzo ya Kiufundi na Teknolojia Dkt Esther Muoria wakiwa ktika Nyeri National Polytechnic.** PICHA: WANGARI MWANGI

KEFEP ulizinduliwa 2016 kwa lengo la kuimarisha Vyuo vya kiufundi kama vinavyochangia pakubwa kufanikisha Ajenda Nne Kuu, Ruwaza ya 2030 na kutimiza Malengo ya Maendeleo Endelevu. Mradi huo unafadhiliwa na Serikali ya Canada kupitia Global Affairs Canada (GAC) na kutelezwa na and Institutes Canada (CICA Colleges N) kutia nguvu ubora wa mipango ya mafunzo ya ujuzi inayozingatia usawa wa jinsia na kutoa wanafunzi wanaotimiza mahitaji ya soko la sasa la ajira. Maeneo ya kuangazia ni Kilimo, kawi, uhandisi, ujenzi, ukarimu na Utalii.Kwa upande wake Gavana wa Nyeri

Mutahi Kahiga alisifu taasisi hiyo kwa kuzamia sekta ya maziwa na akasema serikali ya kaunti inasubiri kwa hamu kutumia ujuzi wa kituo hiyo kuimarisha sekta hiyo.

# Taasisi yazindua mpango wa kulisha watoto 3,500 shule za Kwale na Kilifi

NA HUSSEIN ABDULLAHI (KNA)

Kampuni ya kutengeneza vyuma na simiti ya Devki Group, itashirikiana na serikali ya kitaifa kulisha wanafunzi zaidi ya 3,500 wa shule za msingi katika kaunti za Kwale na Kilifi ambao wanaweza kuacha masomo shuleni wakati wowote kutokana na ukosefu wa chakula. Mchango wa chakula shuleni katika kaunti hizi mbili za Pwani utapitishwa kupitia kampuni ya Simba Cement Ltd, ambayo ni sehemu ya Devki Group, iliyoko Bondora kaunti ndogo ya Kaloleni.

Tayari, kampuni hiyo ya simiti imezindua mpango wa lishe kwa wanafunzi zaidi ya 1,000 katika kaunti ndogo ya Kaloleni.

Akihutubia wanahabari akiwa Kaloleni, Bw Peter Paul, ambaye ni Mkuu wa Usimamizi wa Devki Group alisema kwamba hatua hiyo ni sehemu ya kampuni hiyo ya kuwajibika kwa jamii (CSR).

Bw Paul anasema kwamba kukabiliana na ukame kwa njia ya mpango wa lishe shuleni katika maeneo yaliyoathiriwa zaidi ya kaunti hizo mbili kutafanya watoto kubaki shuleni kufuatia ripoti kwamba mamia wanaacha shule kusaidia wazazi wao kutafuta chakula.



**Peter Paul, afisa mkuu msimamizi Devki Group of Companies akabidhi wanafunzi wa Maereni Primary School, Kilifi mseto wa bidhaa alipozindua mpango wa lishe shuleni.**
PICHA: HANIEL ALEMAYEHU

"Tunapitia nyakati ngumu sana ikizingatiwa kwamba mvua haijanyesha kwa misimu minne mfululizo na hii imetufanya tuamue kutoa chakula kwa shule na makao ya mayatima," alisema afisa huyo wa kampuni.

Bw Paul anaongeza kuwa kampuni itashirikiana na serikali za kaunti hizo mbili za Kilifi na Kwale kuzisaidia kukabiliana na mzozo wa kibinadamu unaokumba wakazi na wanafunzi. Mbali na mpango wa lishe shuleni, Bw Paul anasema Devki Group itaanza mpango wa kusambaza maji kwa malori maeneo yaliyoathiriwa mno na ukame ili kuokoa maisha ya watu na mifugo wao wachache waliobaki.

"Ninataka kumshukuru mwenyekiti wa kundi la makampuni ya Devki Dkt Narendra Raval na Bodi ya Wakurugenzi kwa kukubali kusaidia jamii katika maeneo haya wakati wako kwa shida kubwa," akasema afisa huyo. Maafisa wa Elimu wanasema kwamba hatua za kampuni hiyo ya kutengeneza simiti itafaa huku ripoti zilionyesha kuwa hali ya ukame ni mbaya hivi kwamba katika sehemu za kaunti za Kilifi na Kwale zinarekodi asilimia 70 ya watoto wanaohudhuria masomo.

Kwa mfano katika shule ya msingi ya Maereni, Kaloleni, Kaunti ya Kilifi, ni watoto 259 wanaohudhuria masomo kila siku licha ya kuwa na jumula ya wanafunzi 370 na hali ni sawa katika shule ya msingi ya Mbungoni iliyo na wanafunzi 550. Kundi ya Makampuni ya Devki ilitoa msaada wa magunia ya Mahindi, maharagwe, mafuta ya kupikia, chumvi na bidhaa zingine zinazotosha kulisha wanafunzi kwa miezi miwili ijayo.

# Tumieni mazingira ya kidijitali kubuni kazi, Owalo aambia vijana



**Waziri wa Habari, Mawasiliano na Uchumi Dijitali Eliud Owalo wakati wa uzinduzi wa Jitume Digital Lab katika Thika Technical Training Institute, Kiambu Alhamisi**

NA MUOKI CHARLES (KNA)

Waziri wa Habari Mawasiliano na Uchumi Dijitali Eliud Owalo amehimiza vijana kutumia fursa iliyotolewa na serikali kuunda nafasi za kazi. Waziri alisema kwamba serikali imetoa majukwaa kadhaa, ikiwemo maabara za dijitali za Jitume, Vituo vya ubunifu vya maeneo bunge na upatikanaji wa intaneti kote nchini kusaidia vijana kupata ujuzi wa ICT na kujipatia riziki. Akizungumza baada ya kufungua Maabara ya Dijitali ya Jitume katika Taasisi ya Mafunzo ya Kiufundi ya Thika kaunti ya Kiambu , Owalo alisema kwamba maabara 17 za Jitume tayari zimeanzishwa na kuunganishwa kote nchini na akaongeza kuwa lengo lao ni kuwafunza wanafunzi milioni moja kozi za biashara na ICT bila malipo ambazo zitawezesha kupata kazi. Owalo aliongeza kuwa serikali pia itaunganisha vijana na kampuni za tekinolojia ulimwenguni wapate kazi za dijitali. "Maabara hizi za Jitume zitawafunza vijana ujuzi wa dijitali na kujenga uwezo wao. Zimeundwa kupatia taasisi za kiufundi kote nchini kompyuta 23,000. Kupitia mpango huu, tunatarajia kuwafunza wanafunzi milioni moja kozi zinazohusiana na biashara na ICT ambazo zinahitajika sana kwa ajira bila malipo," alisema Owalo.

Majukwaa mengine yanayohusiana na ICT yanayotolewa na serikali kuwezesha vijana kupata ujuzi wa dijitali ni Mpango wa Ajira Dijitali ambao Waziri alisema walikuwa wamefunza vijana 73,000 kufikia Desemba mwaka jana.






# Kampuni za kibinafsi kupatiwa leseni ya kujenga mabwawa

NA MUOKI CHARLES (KNA)

Serikali hivi karibuni itatoa leseni kwa kampuni za kibinafsi na watu binafsi kujenga mabwawa na kuuzia maji kampuni za kuyasambaza katika juhudi za kutatua uhaba wa bidhaa hiyo nchini.

Mwenyekiti wa Bodi ya Kuthibiti Huduma za Maji (WASREB) Prof Simon Gicharu alisema kwamba hatua hiyo itapiga jeki usambazaji wa maji na kumaliza uhaba unaosababishwa na ukame wa muda mrefu na mabadiliko ya tabia nchi ambao umefanya vyanzo vya maji kukauka kote nchini.

Akizungumza katika mkutano ambao Kampuni ya Maji na Maji taka ya Thika (THIWASCO) ilipatiwa leseni ya kuhudumu kwa miaka minane ijayo, Prof Gicharu alisema kwamba mpango huo pia



**Mwenyekiti wa Water Services Regulatory Board (WASREB) Prof Simon Gicharu akiongea na waandishi mjini Thika.**

itapunguzia serikali presha ya kuwekeza mabilioni ya pesa kujenga mabwawa makubwa ilivyokuwa ikifanya kwa miaka mingi iliyopita. “Kupitia mpango huo, tutakuwa na mabwawa mengi na hakutakuwa na kisingizio cha uhaba wa maji katika sehemu yoyote ya nchi,” alisema.

Alisema kwamba hatua zitachukuliwa kuhakikisha hifadhi za maji zinajengwa kwa njia ya utaalamu kuzuia visa vya kuvunja au kupasuka kunakoweza kuweka wakazi kwenye hatari.

“Hatuwezi kupoteza maji yanayoenda katika bahari mvua inaponyesha kwa kutarajia serikali itajenga mabwawa yote. Serikali sasa italazimika kuangazia kuweka pesa za mabwawa katika mambo mengine,” alisema. Wakati huo huo, Serikali imepatia leseni Shirika la Ustawi wa Maji la Athi kuwa msambazaji mkubwa wa maji katika juhudi za kuimarisha usambazaji wa maji na usimamizi kote nchini.

Katika mpangilio huo mpya, kampuni ya maji ya Athi itasimamia bwawa la Karimenu II Dam, kiwanda cha kuwekea maji dawa na mabomba ya kusambaza maji kwa kampuni za huduma za maji.

# Wizara ya Fedha yaunda tovuti ya bajeti kuinua uwazi

NA MWANDISHI WA MYGOV

Wizara ya Fedha na Mipango ya Uchumi imeunda awamu ya kwanza ya tovuti yake bajeti, na kufungua njia ya kupatikana kwa urahisi stakabadhi za bajeti na habari zinazohusiana nayo za Wizara, Idara na Mashirika yote (MDAs). Kulingana na Mshirikishi wa Afisi ya Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma Julius Mutua, kuundwa kwa tovuti ya bajeti kumekitwa katika sehemu ya pili ya Mkakati wa Mageuzi ya PFM 2018-23 “ Mkakati na Uwazi katika matumizi kuhusiana na Uwekezaji wa Umma na Utoaji wa Huduma, inayoanzisha ajenda ya wazi ya uwazi wa bajeti ikilenga kuhakikisha kushiriki kwa umma katika mchakato wa kutayarisha bajeti.

Kuundwa kwa tovuti hiyo ni kunaweka wazi matokeo (DLR) chini ya mpango wa GESDeK ( Utawala wa kuwezesha utoaji wa huduma na uwekezaji wa umma Kenya), unaofadhiliwa kwa pamoja na Benki ya Dunia na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD). Baada ya kukamilika kwa awamu ya kwanza, Ajenti Huru wa Uthibitishaji (IVA) inavyohitajika chini ya mpango wa GESDeK, atafanyia tovuti hiyo uchunguzi huru kuthibitiaha inavyofanya kazi. Kulingana na Mkurugenzi wa ICT wa Wizara ya Fedha, Lynne Nyongesa, kuundwa kwa tovuti hiyo ni sehemu ya kampeni ya dijitali kuongeza uwazi, kuinua ushiriki wa umma katika kutayarisha bajeti, kuimarisha uwajibikaji katika ufanyaji maamuzi yanayohusiana na usimamizi wa pesa za umma.”

“ Awamu ya kwanza ambayo imeundwa, inahusu kuundwa kwa tovuti kwa kuanzisha mifumo ya usimamizi wa data ili umma uweze kupata data za bajeti za mipango na mipango midogo wakizitafuta.”

“Umma utaweza kupata habari kuhusu jinsi pesa za umma zinatumiwa shuleni na hospitalini,” aliongeza.

Tovuti hiyo ya bajeti iliyoundwa na timu ya maafisa wa ICT wa wizara tofauti, inaweza kupatikana kupitia *https://bajetiyetu.treasury.go.ke* .

# Kaunti ya Murang’a yapitisha sera ya kuinua kilimo hai

NA ANITA OMWENGA NA LAWRENCE MUNYAKA (KNA)

Serikali ya Kaunti ya Murang’a kwa ushirikiano na Taasisi ya Utamaduni na Ekolojia (ICE) na washirika imepitisha kuwa sheria Sera ya Kilimo kolojia

Murang’a 2022-2032 na Sheria ya Kilimo ekolojia ya kaunti ya Murang’a, 2022.

Sheria hiyo inainua matumizi ya mbinu za kilimo hai na uzalishaji wa bidhaa za kilimo hai. Kaunti hiyo inatambua kwamba kwa kula chakula chenye afya, wakazi watakuwa na maisha mazuri na yenye afya. Akizungumza katika hafla ya kuzindua na kutia saini sheria hizo katika uwanja wa michezo wa Ihura mjini Murang’a, Naibu Gavana Stephen Munania alisema sera na sheria ya Kilimo ekolojia kaunti ya Murang’a, zimetungwa kutoka sheria, maendeleo na kuinua sekta ya chakula salama katika kaunti hiyo.



**Naibu Gavana wa Murang’a Stephen Munania alipotembelea mojawapo ya vibanda kuonyesha bidhaa hai wakati wa uzindui wa mpango wa ACT.** PICHA: ANITA OMWENGA

“Wakazi watanufaika na elimu katika kilimo hai ili kuhakikisha bidhaa zao sio tu zenye afya mbali pia zinaweza kuuzwa kote ulimwenguni, katika nchi ambazo zinategemea bidhaa za kilimo hai kila siku kwa kilimo endelevu,” alisema Munania.

Naibu Gavana huyo alisema kwamba chini ya uongozi wa Gavana Dkt Irungu Kang’ata, serikali ya kaunti itahakikisha kuwa wakazi watanufaika katika mfumo kazi wa miaka kumi unaonuiwa kuhakikisha kuwa kilimo hai kitaendelezwa katika kaunti hiyo.

Alisema kwamba kupitishwa kwa Sheria hizo mbili kumeweka kaunti hiyo kuwa miongoni mwa wadau waliojitolea kuwa na mifumo kazi ya kisheria ya kuongoza utekelezaji wa mbinu za ekolojia kilimo, ambazo zitasaidia uzoefu wa mabadiliko ya tabia nchi na mifumo endelevu na stahimilivu ya chakula. “Kaunti inalenga kuwa Kituo cha ubora cha kilimo ekolojia na kuinua ulaji wa chakula chenye afya miongoni mwa watu wake,” alisema, na kuongeza kuwa sera na sheria ya K

Kilimo ekolojia ya Murang’a ni ya kwanza kupitishwa nchini Kenya. “Kwa kutia saini sera ya kilimo ekolojia na sheria, tunaonyesha tunajali watu wetu kwa kuwa itahimiza wakulima kupanda mimea yenye afya na hivyo basi kupunguza gharama ya matibabu,” alisema. Aliomba kila mkazi wa Murang’a kuzingatia Sheri hiyo akisema kwamba kwa kufanya hivi, kutawezesha kaunti kuinua njia za kilimo ekolojia za uzalishaji na uuzaji wa chakula.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utamaduni na Ekolojia (ICE) Martin Muriuki alisema kwamba taasisi hiyo imeshirikiana na serikali ya kaunti kutoa mchakato wa kutayarisha sera na sheria ya kilimo ekolojia.

“Tumeshirikiana na wadau wengine katika Murang’a kujenga uwezo wa wakulima na jamii kupitia ushirikishi wa umma ili sheria hii ipitishwe,” alisema, na kuongeza kuwa itainua kilimo endelevu, kulinda mazingira na kuimarisha utoshelevu wa chakula katika kaunti hiyo.

# Serikali yatwaa mpango wa Tusome kutoka USAID

NA DOUGLAS NAMUNANE (KNA)

Serikali sasa itasimamia ufadhili na utekelezaji wa Mpango wa Tusome kufuatia kuhamishwa kwa majukumu hayo kutoka kwa Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Amerika(USAID) hadi Wizara ya Elimu.

Tangu ulipoanzishwa 2014, mpango huo umekuwa ukifadhiliwa na

USAID kwa usaidizi wa kiufundi kutoka taasisi ya Research Triangle Institute.

Tusome ni shughuli ya kusoma ya gredi za kwanza ulioanzishwa kuimarisha uwezo wa kusoma wa wanafunzi katika shule za msingi za umma nchini.

Kuhamishwa kwa majukumu kutoka USAID hadi Wizara kulifanyika katika hoteli moja ya Naivasha.

Mkurugenzi wa Elimu ya Msingi katika Wizara ya Elimu Bi Nereah Olik aliyeongoza hafla hiyo alisifu mpango huo akisema umeleta mabadiliko yaliyowezesha serikali kuharakisha kila mwanafunzi Kenya anapata vitabu vya kiada katika shule zote za msingi nchini.

Kabla ya mpango huo, hatukuwa na vitabu katika shule lakini kwa wakati huu nenda katika kila shule ya msingi iwe iko Turkana, Lamu au Busia utapata kila mwanafunzi anatumia kitabu chake,” alisema Bi Olik.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa kupitia Tusome, Wizara imeweza kukumbatia ununuzi wa pamoja wa vitabu, na kurahisisha usambazaji shuleni.

Mkurugenzi huyo pia aliorodhesha kufanywa dijitali kwa vifaa vya kufuatilia masomo kama ufanisi mwingine wa mpango huo.

“sasa hivi, nikienda katika shule ya msingi ya Longonot, nitaweza kufanya utathimini na chochote ninachofanya kitanaswa katika wizara ya mara moja. Hii imesatusaidia katika wizara kutotumia makaratasi zaidi ya kufanya maamuzi kwa sababu habari zinapatikana,” aliongeza Bi Olik.

Alisema kwamba mfumo huo umerahisishia wizara kubaini shughuli za kila siku katika shule.

Mkurugen zi huyo alisema kwamba mpango huu wa Tusome umetekeleza jukumu muhimu la kuwezesha masomo yaliendelea hata baada ya shule kufungwa katika kipindi cha mlipuko wa COVID-19.

Hii ni kwa sababu kila mwanafunzi alikuwa na vitabu vya kila somo ambavyo alitumia kusoma akiwa nyumbani shule zilipofungwa kipindi cha janga hilo.

“Sote tunajua kilichofanyika mwaka wa 2020 wakati COVID - 19 ilikuwepo. Shule zote zililazimika kufungwa. Hata hivyo, tunajivunia kwa sababu wanafunzi wetu waliendea na vitabu nyumbani na waliweza kutangamana na vitabu katika kiwango cha kibinafsi,” alisema Bi Olik.

MyGov.
MACHI 14, 2023
NAIROBI-KENYA I TOLEO No. 35/2022-2023

A PUBLICATION OF
**Government Advertising Agency**
Telposta Towers, Kenyatta Ave/ Koinange Street
P.O Box 30025-00100,
Nairobi Kenya
Telephone: (+254) 4920000 / 1
E-Mail: info@information.go.ke

# Majadiliano mbioni kuinua uzalishaji avokado na maharagwe ya kifaransa

**NA BERNADINE MUTANU (MYGOV)**

Huku wakulima wa mboga na matunda wakijitahidi kuhimili athari za janga la Covid-19 na ukame, wadau wanafanya mazungumzo katika juhudi za kuinua mifumo ya thamani ya avokado na maharagwe ya kifaransa. Mazungumzo yanaendelea kutayarisha sera zitakazosaidia wakulima katika mifumo hii ibuka na muhimu ya thamani katika sekta hiyo, mojawapo ya zinazoongoza kuletea Kenya pesa za kigeni.

Mifumo hiyo miwili ya thamani iliathiriwa vibaya na janga hilo, huku wakulima wa mashamba madogo wakipata hasara kutokana na ukosefu wa usafirishaji, huduma za nyanjani na pesa za kununua pembejeo za shambani. Utafiti uliofanywa na Kituo cha Ujasiriamali wa Kibaiyolojia Afrika (CABE) kwa ushirikiano na Taasisi ya Masomo ya Maendeleo (IDS) mwaka wa 2021 inaonyesha kuwa maelfu ya wakulima wa mashamba madogo wa avokado na maharagwe ya kifaransa huenda walipata hasara kubwa. Basdhi ya masuala makuu yaliyoangaziwa katika utafiti huo ni viwango vya juu vya mabaki (MRLs) katika maharagwe ya kifaransa na uvunaji wa avokado kabla ya kukomaa.



Dkt Hannington Odame, Mkurugenzi Mkuu wa CABE, akifafanua jambo kwa washikadau mjini Bomet.

Kulingana na Dkt Hannington Odame, Mkurugenzi Mkuu wa CABE, ripoti ya utafiti huo na mafunzo yaliyopatikana yanaweza kutumiwa kuandaa sera ya ustahilimivu wa mifumo ya chakula wakati wa mizozo ikiwemo mabadiliko ya tabia nchi na majanga. Katika warsha ya kuthibitisha utafiti iliyofanyika Kimana, kaunti ya Kajiado , wakulima wa maharagwe ya kifaransa walisema kwamba ingawa ni tatizo, tatizo kubwa zaidi ni soko, kabla na baada ya Covid-19.

Sammy Chebochok, mkulima na mwanachama wa Chama cha Ushirika cha Friends of Kilimanjaro Initiative (FOKI) , alisema ingawa wako na uwezo wa kuzalisha tani 50 hadi 70 za zao hilo, hawafanyi hivyo kwa kukosa soko. "Bado hatuzalishi tunavyopaswa. Badala ya kuzalisha tani 50 hadi 70 tunazalisha tani 25 kwa wiki. Tunakumbwa na changamoto ikiwemo uhaba wa maji juu ya ukweli kwamba baadhi ya kampuni zinatumika kama mabroka," alisema. Wakulima hao hufanya kilimo kwa kandarasi na anayewauzia nje ya nchi anaweza kuchukua sehemu ya zao lao na kuacha inayobaki kuharibiwa, na hivyo basi wakulima kupata hasara.

"Pia ni vigumu kufuatilia mkulima katika mchakato wa kushughulikia zao. Wakati mwingine zao hukataliwa kwa wingi jambo ambalo linavunja moyo," alisema na kuongeza kuwa wakulima wanafaa kuwakilisha katika sehemu za upakiaji ili kubaini kiwango cha zao linalokataliwa.

"Covid-19 ilipokuja, iliituathiri sana kwa kuwa hatukuitarajia. Wakulima na wasafirishaji hawangekutana kwa sababu ya marufuku ya usafiri," alisema.

# Wanafunzi 1,200 kunufaika na mpango wa ulezi wa masomo ya STEM Machakos

**NA ROSELYNE KAVOO (KNA)**

Karibu wanafunzi 1,200 kutoka shule za sekondari kaunti ndogo ya Machakos watanufaika na mpango wa ulezi wa masomo ya Sayansi, Tekinolojia, Uhandisi na Hisbati (STEM) kwa hisani ya Kituo cha Elimu ya Hisbati, Sayansi na Tekinolojia Afrika (CEMESTEA).

Mshirikishi wa Mipango Spesheli na Masomo ya Wanafunzi katika CEMESTEA Beatrice Macharia alisema kwamba zoezi hilo la siku nne katika shule ya sekondari ya Katoloni ni miongoni mwa mipango inayoendeshwa na Shirika hilo la serikali kuimarisha utendaji katika elimu ya STEM.

Unajumuisha kujenga uwezo wa walimu kuhusu maudhui na ufahamu katika elimu ya STEM na kuunganishwa na ICT.



Mkufunzi kutoka Centre for Mathematics, Science and Technology Education in Africa (CEMESTEA) aelezea jambo kwa wanafunzi wa Katoloni Secondary School.

Akizungumza katika shule ya Katelembu, mshirikishi huyo wa mipango spesheli na masomo ya wanafunzi alisema kwamba zoezi hilo litatoa nafasi kwa wanafunzi na walimu kutangamana na wakufunzi wa CEMESTEA na kunufaika na rasilmali na shughuli za STEM katika shule zao.

"Shughuli hizi zinalenga kumotisha wanafunzi kufaulu katika masomo ya STEM na kazi kupitia ziara katika shule. Katika Machakos, tutakuwa katika shule za sekondari zaKatoloni, Katelembu, Katheka Kai na Machakos," akaongeza Macharia.

Aliongeza kuwa mpango huo ulianzishwa Septemba mwaka jana na kufikia sasa umeendeshwa kaunti za Nairobi na Nakuru.

"Lengo letu ni shule za kiwango cha kaunti ndogo ambazo huenda hazina rasilmali mali za kutosha za STEM na vifaz au shule ambazo huenda hajawahi kuwa na fursa ya kutembelea kituo chetu cha ubunifu katika CEMESTEA," alisema mshirikishi huyo. Bi Macharia alisema kupitia mpango huo, CEMESTEA imeweza kutambua mapengo katika elimu ya STEM ambayo yatashughulikiwa wakati wa mafunzo ya walimu.

"Mapengo ambayo tunatambua yataongoza maandalizi ya mpango utakaotumiwa kufunza walimu wa STEM," aliongeza.

## KWA UFUPI

### Kaunti, USAID kufunza maafisa wa ushirika

Serikali ya Kaunti ya Nakuru na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Amerika (USAID) zimeshirikiana kuwapa mafunzo maafisa kutoka vyama saba vya ushirika vya kahawa kwa lengo la kuimarisha usimamizi na uwajibikaji katika sekta hiyo. Afisa Mkuu wa ushirika katika kaunti hiyo Martin Kagai alisema kwamba kaunti pia inashirikiana na serikali ya Kitaifa kutia nguvu vyama vya ushirika kama chombo pendwa cha maendeleo na akaongeza kuwa usimamizi bora, ubunifu na matumizi ya mbinu bora ni muhimu kwa kuendeleza ukuaji wa vyama vya uushirika. Akizungumza alipofungua rasmi mafunzo hayo katika kituo cha vijana cha Kenya Assemblies of God (KAG) eneo la Maili Sita, Kagai alisikitika kuwa vyama vya ushirika vimekumbwa na matatizo ya usimamizi na kusababisha wanachama kupoteza mamilioni ya pesa kupitia wizi unaotekelezwa na maafisa na maamuzi mabaya ya uwekezaji.

Mafunzo hayo yaliyofanywa na kituo cha Ukuzaji wa Biashara Ndogo Kenya cha USAID (Kenya SBDC) yalivutia viongozi kutoka vyama vya ushirika vya Jumatatu, Solai, Ndemu, Mutungati, Mandizi, Kiremba na Wikurie.

Vituo ya Ukuzaji wa Biashara Ndogo Kenya (Kenya SBDC) ni mpango wa miaka mitano unaofadhiliwa na USAID na kutekelezwa na Chuo Kikuu cha Strathmore. Afisa Mkuu huyo alisema kwamba usimamizi mbaya katika vyama vya ushirika vya kilimo unaathiri mapato ya familia, na pia ni tisho kwa utoshelevu wa chakula na lishe na pia unalemaza ukuaji wa uchumi.

Hata hivyo alifurahia kwamba kupitia ushirikiano huo wa mafunzo, vyama vingi vimekuwa kuwa kubwa na kupanua biashara zao zaidi ya jukumu la kimsingi la kuuza mazao ya wakulima wadogo na kuanza kutoa huduma za fedha. Kupitia mafunzo hayo, Kagai alisema, viongozi hupata ujuzi, ufahamu na kujua kufanya maamuzi ya kufaidi vyama vya ushirika na wanachama wake.

"Mafunzo hayo yameundwa kusaidia viongozi kutoa mazingira bora ya usimamizi bora. Yatapatia mameneja na wafanyakazi nafasi ya kulewa hali ya kipekee ya biashara ya ushirika na mahitaji ya wanachama," akasema Kagai.

*Esther Mwangi na Okello Tracy*

### Mwongozo mpya wa sera TVET kuinua mafunzo ya walemavu

Serikali imeanzisha mwongozo wa sera katika taasisi zote za Elimu yaKiufundi na Mafunzo anuai (TVETs) ili kuinua uafikiaji wa watu walio na ulemavu (PWD) kwa kuwapa ufahamu na ujuzi.

Katibu wa Idara ya Serikali ya Elimu ya Kiufundi na Mafunzo Anuai (TVET) Dkt Easter Muoria, akizungumza katika shule ya watu walio na matatizo ya kuona ya Machakos, katika sherehe ya kutoa ufadhili wa masomo na kuanzisha vifaa vilivyotolewa na Toyota Kenya, alisema, ufahamu na ujuzi unaopatikana utasaidia watu walio na ulemavu kushindana na walio na uzima wa mwili katika utafutaji wa kazi kwa usawa.

"Ushirikishi katika mafunzo unanuiwa kumaliza kutengwa kwa watu walio na mahitaji spesheli na walio na ulemavu katika ajira na kupunguza gharama ya uchumi jamii kwa watu binafsi na jamii kwa jumula," alisema Katibu.

Muoria aliongeza kuwa Wizara ya Elimu iliunga kuunganishwa kikamilifu, ambako wanafunzi walio na ulemavu wanasajiliwa katika taasisi tofauti za elimu.

Aliongeza kuwa serikali imeanzisha taasisi nne za mafunzo ya kiufundi kwa wanafunzi walio na mahitaji spesheli kama Taasisi ya Walio na Matatizo ya Kuona ya Machakos, Taasisi ya Kiufundi ya Viziwi ya Karen, Taasisi ya Kiufundi ya Viziwi ya Sikri na ya vipofu iliyo Oyugis na Taasisi ya Viziwi ya St Joseph iliyoko Nyangoma.

"Zaidi ya wanafunzi 2,500 wamejiunga na taasisi nilizotaja hapo juu tangu 2020," aliongeza Katibu Muoria.

Muoria alisema kwamba Idara ya Serikali ya TVE inafahamu kwama taasisi za walemavu hazina uwezo wa kusajili wanafunzi wote wanaohitumu kujiunga navyo kuimarisha mafunzo yanayojumuisha wote.

Hata hivyo, alisema, wanapanga kuwa na miundomsingi ya TVET itakayowezesha walemavu kutumia na kutoa vifaa vya usafi kwa wanafunzi wa kike.

Dkt Muoria aliongeza kuwa kuna haja ya kupanua miundomsingi, kubadilisha mtaala, kujenga uwezo wa wakufunzi na kuongeza ufadhili ili kuinua elimu kwa walemavu. Vile vile, katibu alisema idara ya serikali inatayarisha mtaala, ambao wanafunzi wa TVET watapata asilimia 70 ya mafunzo katika viwanda na asilimia 30 katika taasisi.

*Anne Kangera na Esther Kioko*

REPUBLIC OF KENYA
GAA GOVERNMENT ADVERTISING AGENCY
KENYA YEARBOOK EDITORIAL BOARD
DESIGN AND EDITING OF MYGOV WEEKLY BY THE KENYA YEARBOOK EDITORIAL BOARD
NHIF Building , 4th Floor, P.O. Box 34035-00100
Tel: 0202715390 / 0757029456
Email: info@kenyayearbook.go.ke
www.kenyayearbook.co.ke